# Hati ya Vidokezo kwa Washirika kuhusu COVID-19

The Department of Children, Youth, and Families (DCYF) ilisasisha hati hii ya vidokezo mnamo Mei 27, 2020. DCYF itaendelea kusasisha hati hii kama inavyohitajika. Kwa maelezo zaidi tembelea **dcyf.wa.gov**

Ili kuzuia kuenea kwa virusi vya COVID-19, DCYF ilifunga kumbi za umma katika majengo yetu yote na haifanyi shughuli za ana kwa ana.

**Vifaa vya Kinga ya Kibinafsi (PPE)**

- Hivi ni pamoja na glavu, barakoa, gauni, buti na barakoa za uso.
- DCYF ilipokea PPE na inavitoa kwa vituo vinavyohudumu saa 24 kila siku na kwa wafanyakazi ambao wako katika hatari ya kuambukizwa virusi vya COVID-19. Tunajua kwamba PPE zaidi vinahitajika, na tunajitahidi kupata vingine.

## Mipango ya Msaada kwa Familia

**Kutembelea Manyumbani**

- Mnamo mwezi Machi, DCYF iliwaomba watoa huduma wa kutembelea nyumbani kusimamisha ziara za ana kwa ana na kutoa huduma za video au ya simu badala yake. Ziara pepe zinaweza kuendelea hadi Juni 30. Baadhi ya watoa huduma za kutembelea nyumbani hutumia ziara za video au ziara za wavuti na simu, barua pepe au maandishi. Baadhi ya watoa huduma wanasafirishia familia vifaa, bila kutangamana nao.
- DCYF iliomba mipango inayofadhiliwa na Home Visiting Service Account (HVSA) isimamishe ziara za ana kwa ana hadi Juni 30.
    - Katika kipindi hiki, DCYF italipia gharama zote sahihi, hata ikiwa hazijatimiza masharti yote.

**Early Support for Infants and Toddlers (ESIT)**

- Watoa huduma wa uingiliaji wa mapema wanatumia huduma za upigaji simu na video hadi Juni 30, ili ziara kati ya watoto na watoa huduma ziweze kuendelea kwa njia salama.

## Ustawi wa Watoto

**Simu ya uandikishaji**

- DCYF inaendelea kutumia namba ya dharura ya kuripoti dhulma na utelekezaji isiyolipishwa ya saa 24 kila siku ya 1-866-363-4276.

**Matembezi**

- DCYF itaendelea na ziara za ana lakini wakati wa janga la COVID-19, ziara zinaweza kutolewa kupitia ujumuishaji wa ziara pepe na za ana kwa ana.
- Ili kuhakikisha usalama kwa watoto, DCYF inaendelea kuchunguza ripoti za unyanyasaji na utelekezaji wa watoto kwa kutumia ziara za ana kwa ana.
- DCYF iliwaomba watoa huduma kufuata itifaki na mwongozo wa afya ya DOH ili kufanya ziara ziwe salama iwezekanavyo kwa washiriki wote.

**Utoaji Leseni ya Huduma ya Ulezi**

- DCYF iliunda uondoaji wa ada za huduma za ulezi na mchakato wa hali maalum ili kutoa usaidizi kwa mipango na familia.
    - Ikiwa hawawezi kutimiza masharti ya Kanuni ya Usimamizi ya Washington wakati wa COVID-19, watoa huduma za ulezi wanahitaji kuwasiliana na shirika la eneo la utoaji leseni ili kujadili chaguo zinazopatikana.
    - Piga simu kwa 1-888-543-7414 ili upate maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuwa mzazi wa ulezi.
- DCYF iliomba watoa huduma wote kukaa mbali na wengine, kama ilivyobainishwa na DOH na amri ya Gavana.

**Uchunguzi wa Uhalifu**

DCYF ilifanya mabadiliko kwenye uchunguzi wa uhalifu wa ustawi wa watoto na mipango ya masomo ya mapema ili kupunguza muda wa kukamilisha shughuli, ili kuondoa vizuizi kwa njia salama na kutathmini watu ambao wanaweza kutoa huduma za utunzaji wa watoto.

## Huduma za Utunzaji wa Watoto

- Vituo vya huduma za utunzaji wa watoto na watoa huduma za nyumbani kwa familia hawapaswi kuwa na zaidi ya watu 10 kwa kila chumba, ikiwa ni pamoja na watoto na watu wazima. Ikiwa kituo kina nafasi ya kutenganisha zaidi ya kikundi kimoja, wanaweza kufanya hivyo.
- Watu walio katika msatari wa mbele wa kushughulikia dharura na watoa huduma muhimu wanahitaji huduma za utunzaji wa watoto (wauguzi, madaktari, watekelezaji wa sheria, wazima moto, wahudumu wa hali za dharura na wafanyakazi wa huduma za jamii). DCYF inapendekeza watoa huduma wahudumie familia kwenye orodha ya huduma muhimu na watoto walio katika hatari zaidi kwa kuzingatia mahitaji ya jamii.
- DCYF inatoa usaidizi kwa watoa huduma za utunzaji wa watoto chini ya CARES Act. Watoa huduma wanaweza kuomba fedha za ruzuku kabla ya Juni 30 au hadi fedha zitakapoisha kupitia **wacompass.force.com/PP_LoginPage**.

**Ruzuku ya Huduma za Utunzaji wa Watoto**

- DCYF inabadilisha kanuni kwa shughuli ili familia ziweze kupata huduma za utunzaji wa watoto wakati huu.
    - Familia lazima ziidhinishwe upya kwa huduma za utunzaji kila baada ya miezi 12 na kuna mahitaji ya kustahiki. DCYF inafanya kanuni ziwe nyumbufu ili familia ziendelee kustahiki.
    - Familia zinahitaji kuomba upya wakati zinahitajika kufanya hivyo na kuripoti hali na shughuli zao.
    - Tunahimiza familia kuomba upya ili kudumisha ustahiki ili ziweze kupata huduma za utunzaji wa watoto wanapohitaji.
    - DCYF inaondoa ada za malipo ya pamoja za Aprili, Mei na Juni kwa familia zinazopokea Working Connections Child Care. DCYF itawalipa watoa huduma kiasi kamili, ikiwa ni pamoja na kiwango cha msingi na kiasi cha malipo ya pamoja ambacho familia ingelipa.

**Washiriki wa Mpango wa Early Achievers**

- Watoa huduma ambao wanashiriki katika Mpango wa Early Achievers wataendelea kupata tuzo za uimarishaji wa ubora na kiasi cha malipo kulingana na daraja kinachozingatia malipo yao ya uandikishaji. Gavana Inslee alifutilia mbali sheria zinazohusiana na muda na masharti ya Mpango wa Early Achievers ambazo hazitaathiri malipo ya haya.

## Juvenile Rehabilitation (JR)

- DCYF ilibadilisha ziara za ana kwa ana na ziara za video.
- Wafanyakazi na watoa huduma wote wanaoingia katika vituo vinavyofanya kazi saa 24 kila siku sharti wapimwe mapema ikiwa wana dalili za COVID-19.
- Kabla ya kuingia kwenye jengo la JR, wafanyakazi, watoa huduma na wanakandarasi huulizwa ikiwa wametangamana mtu yeyote anayeonyesha dalili.
- Wafanyakazi, wakaazi na wakandarasi wote sharti wanawe mikono yao wanapoingia kwenye vituo.
- Mara kwa mara huwa tunaeua vituo, haswa sehemu zinazoguswa sana.
- Wakazi wote sharti wafahamishe wafanyakazi mara moja ikiwa wanahisi kuwa wagonjwa.
- Ikiwa mtu yeyote anajihisi mgonjwa, wafanyakazi watawasiliana na mtoa huduma za matibabu mara moja na kuwaarifu familia.

## Mawasiliano

Tafadhali tembelea maelezo yetu ya mawasiliano kwenye tovuti ya DCYF au utume barua pepe kwa **dcyf.covid-19@dcyf.wa.gov** ukiwa na swali lolote.

Ikiwa ungependa nakala za hati hii kwa muundo au lugha mbadala, tafadhali wasiliana na DCYF Constituent Relations (1-800-723-4831 | 360-902-8060, **ConstRelations@dcyf.wa.gov**).

DCYF PUBLICATION COMM_0078 (05-29-2020) SWAHILI (Kiswahili) – SI